**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Hamsini na Nne - Tarehe 21 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, kwa niaba yake Mheshimiwa Mangungu.

Na. 437

**Madai Mbalimbali ya Walimu**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. MOSES J. MACHALI)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la kuwalipa Walimu madai yao mbalimbali yakiwemo madai ya matibabu, uhamisho, masomo pamoja na tofauti ya mishahara yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali amepata ajali jana usiku, watu wamemvamia wakampiga, kwa hiyo yupo hospitali, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa pole kwa taarifa hiyo uliyotupa ambayo tulikuwa hatuna.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari Mwaka 2012, Serikali iliidhinisha shilingi bilioni 19.2 za madai yasiyo ya mishahara kwa Walimu walio katika mamlaka za Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya ya Kasulu ilipatiwa shilingi milioni 105 kwa ajili ya Walimu 79. Fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya malimbikizo ya mishahara ziliidhinishwa shilingi bilioni 25.6 na zimekuwa zinalipwa na Hazina kupitia mfumo wa ulipaji wa mishahara katika akaunti za Walimu husika. Hadi kufikia mwezi Mei, 2013, asilimia 97.4 ya Walimu walikuwa wamelipwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa stahili za Walimu kuhusu matibabu, uhamisho, masomo na likizo kupitia mipango ya bajeti ya kila mwaka. Mwaka 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilitengewa fedha za likizo shilingi milioni 155 na uhamisho shilingi milioni 170. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 zimetengwa shilingi milioni 586.6 kwa ajili ya likizo. Malipo ya matibabu hufanyika kupitia fedha za matumizi ya kawaida (*OC*).

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zimeagizwa kuandaa rejista ya madeni ya watumishi kila miezi mitatu zijadiliwe kwenye Kamati za Menejimenti, Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Utawala na hatimaye Baraza la Madiwani ili kujiridhisha kwamba madeni hayo yanastahili na kwamba wanaandaa utaratibu wa kuyalipa. Aidha, msisitizo umetolewa kwa Halmashauri kuwa na mipango ya mafunzo ya orodha ya likizo (*leave roster)* ili kuepusha kuzalisha madeni.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza. Serikali kila mwaka imekuwa ikijitahidi kumaliza madeni haya ya Walimu. Ni lini hasa Serikali itafikia mwisho wa kuondoa huu msamiati wa madeni ya Walimu na watumishi wa kada nyingine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali inafahamu kwamba kuna urasimu usio wa lazima wa watumishi pale ambapo wanakuwa wamemaliza masomo yao kupandishwa vyeo ambapo mzunguko wake ni mrefu, kwenda Utumishi mpaka kuja kurudishwa tena kwenye Serikali za Mitaa na kurudi Halmashauri. Kwa nini sasa Serikali isiweke mfumo ambao itakuwa mtu akimaliza masomo yake apandishwe daraja kwa wakati na apate stahiki zake kwa wakati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kumaliza madeni, ni kwamba ulipaji wa madeni ni suala linaloendelea, kwa sababu likizo wanaenda kila siku na sisi tunalipa, kwa hiyo yatakuwa yakizaliwa yanalipwa. Kwa hiyo, hakuna siku hata moja tutafika tutasema leo wote tumeweza kuwalipa. Cha msingi ni kwamba kila madeni yanayozaliwa yanalipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Watumishi wanaoenda kusoma kubadilishiwa vyeo, inategemea kile alichokwenda kukisomea kama hiyo nafasi ya kumpandisha inawezekana. Siyo kila nafasi unaweza kupandishwa *automatic*.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, imethibitika kuwa Wizara pamoja na TAMISEMI huwa inaandaa utaratibu wa Walimu kulipwa stahiki zao lakini Hazina huwa wanakwamisha malipo ya walimu na walimu wanacheleweshewa malipo yao na kwa kuwa Walimu wengi wamekuwa wakipata matatizo ya kuugua na wanacheleweshewa kupewa pesa kwa ajili ya matibabu tofauti na ilivyo kwetu sisi Wabunge. Je, ni lini sasa

Serikali itahakikisha Walimu na wao wanapata stahiki zao ikiwa ni pamoja na pesa za matibabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa namna alivyoliweka vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili nataka niweke vizuri hapa kwa sababu kundi tunalolizungumza ni kundi kubwa na kama tunavyosema kila wakati madeni yanazaliwa. *It will be very unfair,* kusema kwamba Hazina hawafanyi kazi yao, Hazina wanafanyakazi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya hii ya Kasulu inayozungumzwa hapa asilimia 97 ya madeni yote yalishalipwa kwa maana ya yale yaliyohakikiwa. Kama alivyosema Waziri wa Nchi hapa ina-*accumulate* kila wakati, *we are not static*, ndiyo maana ukizungumza na Ndugu Ulochu atakuambia kwamba anayo orodha ya madeni hapa *which is true,* ni kweli ana madeni pale. Kwa hiyo tumekuwa tunalipa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini imetokea hivi, kwa sababu tumechukua muda mrefu, tumejaribu kujiuliza kwamba hiki kitu kwa nini kinaendelea kutokea? Kinatokea katika mazingira yafuatayo. Kwanza, kama Mwalimu alipangwa kwenda Mtwara hakuenda Mtwara akaenda Magu, tayari tatizo litazaliwa pale, kwa sababu mshahara utaenda Mtwara. Wakikaa watatu, wanne wamekutana hivi hawatakuambia unajua sisi ndiyo wale ambao hatukuenda kule tulikopangwa, wao watanyamaza tu. Nataka nikuhakikishie kwamba tumejaribu na tutaendelea kufanya hivyo, Walimu wote ambao wamepangwa katika maeneo waliyopangiwa wakienda kule hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, la pili, hawa wanaokwenda kwenye masomo, *LAWSON* inayozungumzwa hapa, ukikuta

tu cheti hakipo pale itakataa, haiingizi tayari ni tatizo limetokea pale. Kwa hiyo, mazingira haya ndiyo yanasababisha madeni yanatokea. Kama Mwalimu anakuja huku anasema mimi nilifaulu kumbe kuna somo moja kule hakufaulu itakataa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kama Wabunge wana *genuine cases* zinafahamika kwamba yote hayo tuliyosema yametekelezwa, watuletee hapa waseme kwamba ni hawa tutakwenda kushughulikia wala hatuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bima ya Afya, Bima ya Afya Mkuu haishughulikiwi na kule *centre* kule, Bima ya Afya inashughulikiwa pale Urambo, inashughulikiwa pale kwako Njombe, pale Siha ndipo inaposhughulikiwa. Kwa sababu kuna utaratibu wa Bima ya Afya ambao ni *statutory*. Asilimia tatu mwajiri anakuwekea na wewe unakatwa asilimia tatu inawekwa pale. Kinachogomba hapa ni kwamba akihamishwa mgonjwa yule kutoka Kasulu akapelekwa Muhimbili mtalipa vitu viwili, mtalipa nauli halafu utamlipia na hela ya kujikimu pale kwa wiki moja au wiki mbili kutegemeana na muda atakaokaa pale. Malipo hayo yote yanalipwa kupitia *OC* wala hayapiti kule Hazina, Hazina itakuleta tu pale. Kwa hiyo, sisi tunachoomba kama wana madeni yoyote pale Kasulu kwa sababu Genzabuke anatoka huko ya watu ambao wamekwenda huko na Moses Machali bahati mbaya sasa kuna hilo tatizo limetokea, kama wanayo watupatie hayo madeni tutashughulikia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali limechukua dakika kumi badala ya tano, Mheshimiwa Nchemba uliza kwa kifupi.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua *experience* ya nchi nyingine zikoje. Mheshimiwa Waziri amesema madeni yatakuwa yanazaliwa kila mara. Kwa kuwa tunajua idadi ya Walimu, tunajua wanaokwenda kusoma, tunajua na kila mwaka wataenda likizo, hivi hakuna namna ya ku-*set program* kama nchi zingine wanavyofanya

ili inapofika wakati ule tayari kuwe kumewekwa kwenye bajeti ili kuondokana kabisa na malimbikizo siyo tu kulipa madeni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, tunafahamu idadi ya Walimu ambao wanapaswa kwenda likizo. Kwa mujibu wa sheria zetu ni kwamba baada ya mwaka mmoja mwaka wa pili unapaswa kulipiwa pesa ya likizo. Kwa idadi ya Walimu, ndiyo kusema kila mwaka nusu ya Walimu wanapaswa kuwekewa kwenye bajeti pesa ya likizo lakini tatizo ni uwezo wa Serikali wa kuwalipia wote wanaostahili kwenda likizo kwa mwaka ule.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaliangalia na Vyama vya Wafanyakazi kuona uwezekano kwamba ikiwezekana, kwa sababu haya madeni yataendelea kuwepo kama nilivyotangulia kusema, tunaangalia uwezekano wa kuweka kwenye *LAWSON* ili ikitokea mtumishi anastaafu basi yale madeni yake ambayo hakuenda likizo nayo yaingizwe kwenye pensheni yake. Kwa sababu yote tumejaribu kuangalia bajeti lakini bajeti kuweza kukidhi masomo, matibabu kwa watumishi wote kwa kweli kwa kila mwaka kwa asilimia mia moja ni kitu ambacho tumeona hakiwezekani.

**SPIKA:** Haya muendelee kuangalia, kwani kwa watumishi wengine inakuwaje? Swali linalofuata Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, kwa niaba yake Mheshimiwa Nchemba.

Na. 438

**Uanzishwaji wa Maeneo Mapya ya Kiutawala**

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. AUGUSTINO M. MASELE)** aliuliza:-

Serikali imeanzisha maeneo mapya ya kiutawala ili kusogeza huduma kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kutoa fungu maalum kwa ajili ya maeneo hayo ili kuweza kuandaa mipango miji na kupima viwanja?

(b) Je, Serikali itaanzisha lini Halmashauri za Wilaya mpya na kuteua Wakurugenzi wake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi mwaka 2012/2013, Serikali iliazimia kuanzisha Halmashauri 35 ambapo hadi sasa Halmashauri 35 zimepata *GN*. Namba na kupata vyeti vya kuanzishwa. Aidha, hadi sasa Halmashauri 30 zimekwishaanza rasmi na Halmashauri tano zilizobaki zinaendelea na taratibu za kisheria na kiutawala ili ziweze kuanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuziwezesha Halmashauri kupitia Mfuko wa Mikopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja uliopo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo Halmashauri hukopa na kuweza kuandaa maeneo ya Mipango Miji.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayoikabili Mfuko huu ni Halmashauri kutokurudisha fedha hizo kwa wakati. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inaendelea kuzifuatilia Halmashauri zilizokopa ili ziweze kurudisha kwa wakati fedha hizo ili ziweze kukopeshwa kwa Halmashauri zingine zenye mahitaji kama hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha uandaaji wa Mipango Miji na upimaji wa viwanja katika Halmashauri hizo 30, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ziliandaa bajeti zao kwa kuzingatia vipaumbele vyake ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kiliidhinishwa kwa ajili ya upimaji wa viwanja, uandaaji wa Mipango Miji na uanzishwaji wa Masjala za Ardhi. Kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe imetenga jumla ya shilingi 30,000,000 kwa ajili ya mipango miji. Napenda kutoa rai kwa Halmashauri hizi mpya kutumia fursa ya taasisi za kifedha ambazo zipo tayari kutoa mikopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya Halmashauri 35 zilizoanzishwa, Halmashauri 30 zimeshaanza rasmi na jumla ya Wakurugenzi 30 wameteuliwa. Kuhusu Halmashauri za Wilaya ya Mbogwe, napenda kumthibitishia Mbunge kuwa taratibu za kuanzishwa zimekwishakukamilika hivyo basi uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo utafanyika muda wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa hapo juu, Halmashauri nne zilizobakia zitaanzishwa rasmi hapo taratibu za kisheria zitakapokuwa zimekamilika.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri hizi mpya zilizoanzishwa zinatofautiana kimazingira, baadhi ya maeneo Halmashauri hizi mpya kama ilivyo kwa Mkalama, Mbogwe, Momba, Makao Makuu yake yamewekwa kwenye moja ya kijiji tu, ni vijiji kabisa. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa upendeleo kwenye hizi Halmashauri ambazo Makao Makuu yamewekwa kwenye kijiji tu kimojawapo ambacho hakina jengo la aina yoyote la kisasa ili hizo ziweze kuanza mapema kabla ya zingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubali kwamba kweli mazingira kwa Halmashauri tulizozianzisha kwa maana ya kusukuma huduma

kwa wananchi, nyingine zipo katika hali ambayo ni *remote,* yupo *right* kabisa hicho anachosema wala hatuna ubishi nacho.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kuweka hapa waziwazi, kuhusu suala la kuanzishwa kwa hizo Halmashauri 30 na Wakurugenzi wake tayari zimekwishaanza, tulichofanya ni kwamba wengine wamekwenda katika majengo ya watu binafsi, wengine wamekwenda katika majengo ya zamani yaliyokuwepo ya Halmashauri kwa shida kama anavyosema pale. Ni kweli kabisa kama vile unapofanya kwa mtoto mdogo nyumbani anapozaliwa unamwangalia zaidi kuliko wale wengine wote. Kwa hiyo, hili la kusema kwamba unaweka upendeleo kwa Halmashauri hizi, tutafanya hivyo kwa maana ya kwamba tunakuwa makini *otherwise* usipoangalia vizuri huduma zitashindikana kutoka pale. *Experience* yetu inaonesha kwamba mara nyingi sana tunazitegemea Halmashauri Mama ndizo zisaidie katika kipindi cha mpito.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na jibu ambalo Waziri amelitoa, kwamba wataendelea kuwadai polepole mpaka watakapomaliza, hii inaleta picha ya namna gani kwa Serikali kusema watawadai polepole na wakati Halmashauri hizi kila leo tunasema hapa kwamba tumezirundikia mafungu mengi ya kuweza kutumia huko. Kwa nini Waziri asitoe muda maalum kwamba fedha hizi lazima zirudi zilikochukuliwa kwa muda fulani?

**SPIKA:** Umelielewa swali? Anayedaiwa ni nani?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Halmashauri

**SPIKA:** Na nani?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Augustino linasema, je, Serikali ina mkakati gani

wa kutoa fungu maalum kwa ajili ya maeneo hayo ili kuweza kuandaa mipango miji na kupima viwanja? Jibu la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wanaendelea kuwadai polepole, arudie jibu lake kama alivyozungumza hapo mwanzo ili lieleweke kwa wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Aliporudia kuongea sasa ndiyo tumeelewa anauliza nini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Medeye yupo hapa anasikia kitu tunachosema hapa, akipewa nafasi hapa atasema. Lazima tukiri, huu Mfuko tunaouzungumza hapa unaitwa *Revolving Fund* maana yake ni kwamba Kasulu ikichukua hivi unapeleka Kakonko halafu kesho utapeleka tena Halmashauri ya Mtwara, Mwanza na kadhalika. Ukicheki malipo yale yanavyofanyika, hao wanakwenda kupima viwanja, wakienda kupima viwanja wanapata fedha. Kwa hiyo, tunategemea malipo yale ambayo watapata pale watapeleka kule katika Halmashauri. Sasa anachotuuliza sisi kwamba ninyi kwa nini hamuwapi muda maalum wa kulipa? Tutamwomba Waziri Mkuu hapa, tutazikata hizo hela. Mkituruhusu hapa, tutazikata tu, tunaweza kusema Kasulu kata halafu tunamaliza tunapeleka.

Mheshimiwa Spika, nachoweza kusema hapa, kwa sasa hivi tutakachofanya, tutaandika barua tena kwa Halmashauri na hii nasema kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmashauri yoyote ambayo imechukua hela kwa ajili ya mkopo kwa ajili ya kwenda kupima viwanja, mara moja warudishe hela hapa vinginevyo tutashuka nao jumlajumla. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amemaliza yote. Ziko

Halmashauri tunazowadai na agizo alilolitoa kwa kweli, namshukuru kwa hilo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Clara Mwatuka.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali langu lakini kwa masikitiko nataka nikujulishe kwamba swali hili lililoletwa sio la kwangu, sijauliza habari ya rada hata siku moja. *(Makofi/ Kicheko)*

**SPIKA:** Basi ni swali la Spika, naomba ujibu kwa sababu liko hapa. *(Kicheko)*

Na. 439

**Zawadi kwa Wanaofichua Wezi na Wahalifu**

Serikali kupitia Jeshi la Polisi hutoa zawadi kwa wananchi wanaofichua wezi na wahalifu:-

Je, Serikali itatoa zawadi gani kwa wale wote waliofichua wizi wa fedha katika ununuzi wa rada ya Taifa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge lako, napenda kujibu swali lililopo mbele yetu kuhusu rada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 kama

ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, ni wajibu wa kila mwananchi, popote alipo, kutoa taarifa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama kuhusu utendwaji njama ama nia ya kutenda kosa lolote la jinai. Utolewaji wa taarifa za aina hii, husaidia katika kudhibiti vitendo vya uhalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kulijibu swali hili la Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zawadi zinazotolewa na Serikali kupitia Jeshi la Polisi, hutolewa baada ya kuzingatia masuala mbalimbali ya msingi yakiwemo ukubwa au uzito wa uhalifu uliofichuliwa. Aidha, kwa kuzingatia hili, si kila mwananchi anayemfichua mwizi au anayefichua uhalifu hupewa zawadi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi kutoa zawadi kwa wale wote waliofichua wizi wa fedha katika ununuzi wa rada ya Taifa, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hapakuwepo na wizi wowote wa fedha katika ununuzi wa rada. Isipokuwa iligundulika kwamba, bei halisi ya rada hiyo ilikuwa chini ukilinganisha na fedha ambazo Serikali ililipia. Suala hili limethibitishwa kupitia uchunguzi uliofanywa na Taasisi ya Makosa ya Jinai kule Uingereza *(SFO)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufafanuzi huo, Serikali haioni mantiki yoyote ya kutoa zawadi kutokana na suala hilo. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa rai kwa wananchi wote kushirikiana bega kwa bega na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili kutoa taarifa zozote muhimu kuhusiana na uhalifu hapa nchini kwa sababu ni wajibu wa kila Mtanzania.

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. *(Kicheko)*

Na. 440

**Ziara za Mawaziri Nchini**

**MHE. SAID A. ARFI (K.n.y. MHE. MASOUD ABDALLA SALIM)** aliuliza:-

Je, tabia ya Mawaziri kufanya ziara sehemu mbalimbali za nchi bila ya kushirikisha au kutoa taarifa ni msingi wa utawala bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hufanya ziara katika Mikoa mbalimbali nchini kwa lengo la kufuatilia na kukagua utekelezaji wa kazi na mipango ya maendeleo inayohusu Wizara wanazoziongoza. Wanapofanya ziara hizo, Ofisi zao hufanya mawasiliano na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Ofisi zao zilizoko kwenye Mikoa husika. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Ofisi ya Wilaya iliyopo katika Mkoa huo hushirikiana katika kuandaa na kuratibu ziara ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, Waziri anapofanya ziara Mikoani bila ya kutoa taarifa rasmi ya ziara yake, huo si utawala bora. Hata hivyo, hatuna taarifa yoyote ya Mawaziri wanaofanya ziara Mikoani bila kutoa taarifa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, baada ya kulalamika kwa muda mrefu hapa Bungeni, juu ya tatizo la Kituo cha Polisi cha Kengeja, Jimbo la Mtambile, juu ya uchakavu wake na jinsi kinavyovuja katika hali mbaya sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alifika katika kituo hicho lakini bila kutoa taarifa kwa mlalamikaji au kwa mtetezi yaani Mbunge mhusika ambaye ni mimi

mwenyewe. Sasa Mheshimiwa Waziri unasema wewe huna taarifa, jambo hilo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakipiga kelele mara nyingi. Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika kwamba hawashirikishwi wakati Mawaziri wanapokuwa wanakwenda katika Majimbo yao, mnakwenda kimya kimya. Je, tatizo hili ni lini litaweza kupatiwa ufumbuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa nchi za *APRM, African Peer Review Mechanism,* mpango wa kujitathmini wenyewe kwa utawala bora na kwa kuwa matatizo haya yamekuwa yakijadiliwa katika vikao mbalimbali, mnatuhakikishia vipi sisi Wabunge kwamba katika mpango wenu wa *APRM* na kwa sababu unasema jambo hili ulikuwa hulijui halitaweza kutokea tena? Nashukuru.

**SPIKA:** Waziri wa Nchi, *APRM* Waziri kutokwenda huko.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Waziri anapokwenda mahali, kuna mambo mawili, *inspection* na ziara. Kama hapa ilitolewa hoja kwamba Kituo cha Polisi kiko dhaifu, Waziri alienda pale kwenda kuthibitisha, ajionee mwenyewe hali halisi. Alikuwa anakwenda kufanya *inspection* hakuwa anakwenda kufanya ziara, hakuwa anakwenda kufungua Kituo cha Polisi, alikuwa anakwenda kujiridhisha malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge yanahitaji kushughulikiwa kiasi gani. Sasa kama ni kwenda tu kukiona kituo na kuondoka, Mheshimiwa Mbunge ana mambo mengi, unamwambia tu Mbunge nilikuita hapa ili uone ninavyokagua kituo? Kwa hiyo, mimi nasema kitu muhimu ni kwamba Mheshimiwa Waziri hakutoa taarifa kwa sababu alikuwa anakwenda kufanya ukaguzi ili baadaye aweze kushughulikia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, la pili, umeuliza mpango wa *APRM* kuhusu mambo ya kujitathmini wenyewe katika mambo ya

utawala bora na kwamba jambo hili halitatokea tena. Nataka niseme hivi, halijawahi kufanywa na Mawaziri na kwa hiyo nasisitiza halitatokea tena. Halijawahi kutokea kwa hiyo hatuna sababu ya kusema halitatokea tena, kwa sababu halijawahi kutokea.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kiundani swali langu lilikuwa linafanana sana na aliloliuliza heshimiwa Masoud lakini naomba niliongeze kidogo ili na mimi nielewe zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Kumi, nilitoa malalamiko juu ya Kituo cha Polisi Konde kuhusiana na hali ya majengo yalivyo na niliomba ziara maalum kama Mbunge, Mheshimiwa Waziri aongozane nami akaiangalie ile hali ilivyo. Nafurahi kwamba Waziri alikuja na nilikuwepo Jimboni Konde lakini kama Mbunge sikuwa na taarifa na nilimwona Mheshimiwa Waziri akirudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoomba Wabunge twende na Mawaziri kuona hali halisi, Watendaji hawawezi kumwambia ukweli na uzito wa mambo yaliyopo pale, wanamwogopa kwa cheo chake. Leo Mbunge anayeweza kushauriana na Waziri vizuri anakuja kwenye eneo na hataki kushirikiana naye. Je, hii ni haki na ni utawala bora? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza yeye mwenyewe anakiri kwamba swali lake linafanana na swali la Mheshimiwa Masoud, yote ilihusu malalamiko dhidi ya hali ya Kituo cha Polisi, yalihusu Wizara kwenda kufanya ukaguzi, basi kama nilivyomjibu Mheshimiwa Masoud, Waziri alikwenda kufanya ukaguzi, ni safari ya kiutendaji, alikuwa anakwenda kuzungumza na Watendaji, mbona hali iko hivi? Kwa hiyo, hapakuwa na sababu ya kwamba Mbunge awepo pale anamshuhudia anapofanya *inspection.*

Na. 441

**Usambazaji wa Maji kutoka Chanzo cha Maji Katika Kijiji cha Ihelele**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Je, ni sababu gani inayoifanya Serikali kushindwa kusambaza maji kwenye chanzo cha maji katika Kijiji cha Ihelele pamoja na vijiji vya Nyang'homango, Mbarika, Isesa, Mwagiligili, Mahando, Nyamainza na Mwamboku?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza kwa awamu mpango wa kupeleka maji kwenye vijiji vyote vilivyo kandokando ya bomba kuu la kusafirisha maji kutoka Ziwa Victoria. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, Serikali imeunganisha jumla ya vijiji 39 vilivyopo umbali wa kilomita tano kutoka bomba kuu. Wananchi wa vijiji hivyo wanapata huduma ya maji tangu mwezi Februari, mwaka 2009. Katika awamu ya pili ya utekelezaji, Serikali imeongeza wigo katika utekelezaji ambapo vijiji vyote vilivyopo umbali wa kilomita 12 kutoka kwenye bomba kuu vitaunganishwa. Jumla ya vijiji 100 vimeainishwa kama ifuatavyo:- Wilaya ya Misungwi vijiji 18, Kwimba vijiji 11, Shinyanga vijiji 46 na Kahama vijiji 25. Ujenzi wa kituo cha kuchotea maji katika Kitongoji cha Ihelele umekamilika na tayari wananchi wameanza kupata huduma ya maji. Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwa ajili ya kupeleka katika vitongoji vingine vya kijiji cha Nyang'homango inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2013. Zabuni ya kumpata mkandarasi wa kujenga miundombinu ya kupeleka maji katika kijiji hicho kutoka tenki kubwa la Mabale itatangazwa Julai, 2013. Mkandarasi huyo pia atajenga miundombinu ya maji kwa vijiji vya Isesa, Igenge na Mbarika. Vijiji vya

Mwagiligili, Mahando, Mwamboku na Nyamainza ni kati ya vijiji ambavyo vitatekelezwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kazi ya upimaji, usanifu na kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji 100vilivyoainishwa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya na tungependa kweli maji haya ya Ziwa Victoria yafike Tabora mpaka Dodoma kwa Wagogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni lini Serikali itapeleka maji katika vijiji vya Kasololo na Misasi, Jimbo la Misungwi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu upo mradi mkubwa sana wa kutoa maji Ziwa Victoria kupitia Magu mpaka Mji wa Ngudu. Nilitaka kujua kwa Mheshimiwa Waziri, ni vijiji vingapi vitanufaika na mradi huo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba ni lini Serikali itapeleka maji kwenye vijiji vya Kasololo, ni kwamba katika mpango ambao tumeuanzisha sasa hivi wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo ya Haraka *(BRN),* ule mpango moja ya vipengele ni kutekeleza ile miradi ambayo ina matokeo makubwa na ya haraka. Katika miradi hiyo mojawapo ya kipengele hicho ni kufufua miradi ambayo ilikuwepo ambayo ilijengwa lakini sasa imeharibika na haitumiki, pale huhitaji kutumia fedha za kufanya upembuzi yakinifu, unachotakiwa ni kuanza tu kurudisha ile miundombinu. Huu mradi wa Kasololo, ni moja kati ya miradi hiyo na umeingizwa kwenye huu mpango wa *Big Result Now (BRN).* Mradi huu ukitekelezwa, una matokeo makubwa kwa sababu ututatoa maji kwa Kata tatu ambazo zina vijiji 10 kwa ujumla. Kwa hiyo, utakuwa na *effect* kubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba tutaje ni vijiji vingapi ambavyo vitafaidika na huu mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Magu kwenda Ngudu, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Ndassa kwa sababu anafuatilia sana suala hili la maji na ameshafika ofisini kwetu, ametuletea orodha ya vijiji ambavyo viko kati ya Ngudu na Magu ambavyo vinazidi 25 lakini sasa hivi tuko katika hatua za upembuzi yakinifu yaani wana-*design.* Kwa hiyo, ni vigumu sana kuvitaja vile vijiji kwa sababu ile *design* inatakiwa ionyeshe ni sehemu gani yatapita yale mabomba kwa kuzingatia aina ya teknolojia ikiwemo ya mtiririko kutoka kule Magu. Nina hakika, katika vigezo ambavyo wataalam wetu wanafuata, ni kuhakikisha kwamba mradi ule unapita kwenye sehemu ambayo ina watu wengi zaidi. Kwa maana hiyo, nina hakika hata vijiji vyake alivyotuletea, orodha yake ninayo hapa, vitapata maji katika mradi huo.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika kijiji hicho cha Ihelele pale maji yanapoanzia panaitwa *Smith South Bay.* Kwa kuwa Serikali ya Awamu iliyopita ya Mzee Mkapa ndiyo iliyotoa pesa shilingi bilioni 253. Kwa nini sehemu ile isiitwe *Mkapa South Bay? (Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo ametoa hapa ambayo ni mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Ndassa kwa kufuatilia jambo hili kwa karibu na nipende tu kusema kwamba wakati nimetembelea bomba hili, Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Rage alinipokea kule Ihelele. Kwa hiyo, ni mtu makini sana. Nataka tu niseme kwamba jambo hili tutalipeleka kwenye Serikali na kuona uwezekano wa kubadilisha jina la *Bay* hiyo, inaitwa ghuba, kubadilisha ghuba hiyo kama ambavyo amependekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Eeeh, nani anayebadilishaga majina? Si kila mtu tu? Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh.

Na. 442

**Tatizo la Magugu Maji Ziwa Victoria**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Ziwa Victoria ambalo linategemewa sana kwa shughuli za uvuvi na kuwapatia wananchi kipato, linakabiliwa na tatizo la magugu maji:-

(a) Je, ni nini chanzo cha tatizo hilo?

(b) Je, ni athari gani zimejitokeza za kijamii na kiuchumi kutokana na magugu hayo?

(c) Je, Serikali, ina mpango gani wa kuondoa magugu hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, magugu maji ni mimea inayomea na kuelea majini. Asili ya mimea hii ni kutoka katika nchi za Amerika ya Kati katika bonde la Mto Amazon. Magugu maji yaliingia ziwa Victoria mwaka 1986 kupitia Mto Kagera na madhara yake kuonekana mwaka 1988. Mpaka sasa kuna aina mbili za magugu maji katika Ziwa Viktoria, ambayo ni *Water Hyacinth (Eicahronia Crassipes)* na *Water Chest (Trapa Natas).*

(b) Mheshimiwa Spika, athari za kijamii na kiuchumi zilizojitokeza kutokana na magugu maji ni pamoja na kuziba njia za vyombo vya usafirishaji majini, kuathiri shughuli za kimaendeleo, mfano, uvuvi, umwagiliaji, matumizi ya maji nyumbani na viwandani. Pia, magugu maji ni maficho ya wanyama hatari kama vile mamba, kiboko na nyoka.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Viktoria Awamu ya II *(LVEMP II),* unaotekelezwa na nchi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki, chini ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, unatekeleza mkakati wa Kikanda wa kudhibiti magugu maji ambao ulishapitishwa na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Bonde la Ziwa Viktoria.

Vilevile Wizara ya Maji inashirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Halmashauri za Wilaya 14 zilizoko kandokando ya Ziwa Viktoria na Mto Kagera katika kutekeleza miradi midogo midogo ya jamii ya kudhibiti magugu maji.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumza hapa kwamba, kuna mradi wa kuhifadhi mazingira ambao unashughulika na udhibiti wa magugu maji katika Ziwa Viktoria. Je, hadi sasa ni nini mafanikio ya mradi huu?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa juhudi za nchi zote za Afrika Mashariki, za mpambano wa taizo hili. Je, ni lini hasa tatizo hili linaweza likafikia mwisho? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa kufuatilia sana suala hili ambalo ni muhimu kwa shughuli za uchumi katika Kanda ya Ziwa Viktoria. Kuhusu swali lake kwamba, ni nini mafanikio mpaka sasa hivi; ni kwamba, ziko shughuli mbalimbali ambazo zimeainishwa, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi kwamba, katika Wilaya 14 iko miradi mbalimbali ambayo inashirikisha wananchi ya kuondoa hayo magugu maji.

Mheshimiwa Spika, mradi mmoja ambao ni mzuri sana ni wa kujenga vituo vya kuzalisha wadudu, "Mbawakawa",

ambao wao chakula chao kikuu ni magugu maji. Mpaka sasa tuna Vituo saba na tunatarajia kujenga Vituo vingine 19 katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, na kwamba, ni lini tatizo hili litakwisha. Nadhani hii ni *issue* endelevu; tutaendelea kupambana nalo mpaka kuhakikisha kwamba, haliathiri zile shughuli ambazo tumezitaja za wavuvi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mshama, ulisimama? Haya.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na jibu la Mheshimiwa Waziri, imebidi nisimame. Napenda kujua kwa kuwa, tatizo hili linazuia watu wengi na vijana wengi kufanya kazi zao na shughuli zao za uvuvi, hasa za kujiongezea kipato. Je, katika vituo hivyo, kuna kituo ambacho kitajengwa katika Wilaya ya Misenyi, hasa kule katika eneo la Kanyigo, kule Kashenyi kwa sababu ni sehemu ambayo imeathirika sana na magugu maji?

**SPIKA:** Siku nyingine unasimama kabla, sio baada. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilichukue kwa sababu, katika vituo 19 ambavyo tumeainisha ni vituo vingi ambavyo siwezi kujua mara moja kwamba, anachosema kipo. Lakini kwa umuhimu aliousema, nichukue tukafanye ulinganisho na ikibidi tutashauriana ili kuona kwamba na chenyewe kinakuwepo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Barwany, ulitakiwa ukae jana pale, kusudi uweze kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu. *(Kicheko)*

Anasema kukiwa na *vacuum* kawaida huwa inajazwa. Kwa hiyo, tunaendelea, Wizara ya Nishati na Madini?

Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo? Atakayeuliza kwa niaba yake, Mheshimiwa Vita Kawawa?

**MHE. MBUNGE FULANI:** Eeh, makubwa.

Na. 443

**Wananchi Waliohamishwa Kupisha Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka**

**MHE. VITA R.M. KAWAWA (K.n.y. GAUDENCE C. KAYOMBO)** aliuliza:-

Kwa vile, Kampuni ya *TANCOAL* imekwishapata leseni ya uchimbaji wa makaa ya mawe ya Ngaka:-

(a) Je, ni watu wangapi wamehamishwa kupisha mradi huo na wamelipwa kiasi gani cha fedha?

(b) Je, Kampuni hiyo inachukua hatua gani kuwashirikisha wananchi kutumia makaa ya mawe kupikia na kuchoma matofali, ili kupunguza ukataji miti.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TANCOAL Tanzania Limited,* ilipewa leseni namba *ML 439/2011* ya uchimbaji wa makaa ya mawe tarehe 18 Agosti, 2011 katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 9.98 huko Ngaka, Wilayani Mbinga. Kampuni hiyo inamilikiwa kwa ubia kati ya *NDC* ambayo ina 30% na *Intra Energy Limited* yenye 70%.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza uchimbaji wa madini, Kampuni hiyo ilifanya tathmini ya mali za wananchi waliostahili kulipwa fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe, kwa lengo la kulipa fidia kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji.

Baada ya kazi hiyo kukamilika, jumla ya familia 499 zililipwa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 2.12. Aidha, Serikali, imeamuru Kampuni ya *TANCOAL* kulipa fidia kwa familia 306 zilizokuwa zimesahaulika katika tathmini ya awali.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TANCOAL* inashirikiana kwa karibu na wananchi katika kuhamasisha matumizi ya makaa ya mawe badala ya kuni. Kampuni inakiwezesha kifedha Kikundi cha Wanawake kiitwacho *Mbalawala Womens Group* kinachojihusisha na utengenezaji wa *coal briguettes* kwa matumizi ya nyumbani. Kampuni ya *TANCOAL,* ilinunua mashine ya kutengeneza *coal briguettes* kutoka China na kukipatia kikundi hicho. Kikundi hicho pia, kitajihusisha na ufugaji wa kuku na samaki kwa ufadhili wa *TANCOAL.*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Serikali, imekiri kuwa kuna baadhi ya familia zilisahauliwa kulipwa, lakini pia wale waliolipwa walilalamika kwa Mkuu wa Mkoa kwamba, walilipwa kidogo na eneo wanalopaswa kwenda kuhamia pia, linatakiwa nalo lilipwe na Serikali, kupitia Mkuu wa Mkoa, iliahidi mpaka tarehe 15 Mwezi wa 6, itakuwa imewalipa; mpaka tarehe hiyo walikuwa hawajalipwa. Je, ni lini sasa watakuwa na uhakika wa kulipwa fidia zao?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa, Serikali pia, inataka kupanua barabara inayotakiwa kwenda kwenye mradi wa Mkuju *River* wa *Urani,* Namtumbo na imeweka *X* kwenye nyumba za wananchi hao na hawajui kama watalipwa fidia. Je, Serikali nayo, inaweza kwenda kuwaambia ni lini na wao watalipwa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna familia 306 kama tulivyoeleza zilisahaulika kwenye tathmini ya awali. Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, imefanya ufuatiliaji wa suala hili na kuagiza familia zile ambazo tayari zimeshafanyiwa tathmini mpya kwa viwango vya Sheria Mpya ya Fidia, zitalipwa

wakati wowote kuanzia sasa kwa sababu, kazi ya kuhakiki familia hizo imeshafanyika na taratibu za malipo zinaandaliwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upanuzi wa barabara kwa nyumba zilizowekewa *X* kuelekea kwenye Mradi wa Mkuju, kwa taratibu za Wizara ya Ujenzi, pakiwa nyumba zimewekewa *X* kwa rangi nyekundu, tafsiri yake ni kwamba, nyumba hizo hazitalipwa fidia. Zile zilizowekwa *X* kwa rangi ya kijani zitalipwa fidia kwa mujibu wa sheria.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuwapa matumaini wananchi wa Vijiji vya kule Luanda mpaka kule Tarafa nzima ya Namswea ya kulipwa fidia yao, lakini malalamiko ya wale wananchi kule Luanda sio fidia tu ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira, ni pamoja na mavumbi yanayotokana na makaa yale ya mawe kusambaa karibu katika Vijiji vyote na kuhatarisha afya za wakazi wa maeneo yale.

Je, Serikali, inasema nini ili mgodi huo unapoendelea uweze kufuata Kanuni na Sheria bora za Kuhifadhi Mazingira na kutunza afya za Watanzania, ambazo zinaweza kuathirika wakati wowote kwa sababu ya hali halisi ilivyo katika maeneo ya mgodi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ili kampuni iweze kufanya shughuli za uchimbaji ni lazima ikidhi vigezo vyote kwa mujibu wa Taratibu na Sheria zetu. Kampuni hii, ilikidhi vigezo na ndio maana ikapatiwa leseni ambayo nimeitaja kwenye jibu la msingi, ikiwemo na taratibu za mazingira, kwa maana ya kupata *Certificate* ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, shughuli hii ya uchimbaji katika maeneo ya uchimbaji inahusisha uchimbaji wa ardhi na uharibifu wa hali ya hewa, kwa maana ya vumbi linalotimka katika eneo la uchimbaji na ndio maana Serikali, imeagiza mgodi huu ulipe fidia kwa wananchi walioko karibu na eneo

hili la mgodi, ili waweze kupisha wawe mbali na mgodi uweze kufanya shughuli zake bila kuathiri maisha ya kawaida ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa ndugu zangu wa kule Mbinga, watakapopokea fidia hizi, waweze kuhama, kupisha maeneo hayo ya mgodi, ili shughuli za uchimbaji ziweze kuendelea bila kuathiri afya zao.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, inasemekana kwamba, kampuni hii inachimba mkaa huu na kuupeleka nje ya nchi kupitia Malawi. Je, Serikali, haioni kwamba, kuna umuhimu wa kuwapeleka *TMA* wakawepo kule, ili kuhakiki mapato ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, mgodi huu umeshaanza uzalishaji na kwa kawaida kwa taratibu zetu, sehemu yoyote kwenye mgodi ambapo uzalishaji umeshaanza *TMA* wanakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika eneo la mgodi wa Ngaka, tunao wawakilishi wa *TMA* na malipo ya mrabaha yanalipwa ambayo kwa sababu, makaa ya mawe ni madini ya ujenzi, tunapokea 3% ya malipo ya mrabaha katika kila mauzo yanayofanyika ya makaa ya mawe haya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, si kwamba, makaa ya mawe haya yanapelekwa nje ya nchi, pia yanauzwa ndani ya nchi katika viwanda vya *Twiga Cement,* Kiwanda cha *Mbeya Cement* na viwanda vingine ambavyo vipo hapa nchini, vinavyotumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali, kupitia *TANESCO* wako kwenye mazungumzo na kampuni hii kuweza kutumia makaa ya mawe haya kuzalisha umeme kiasi cha *Megawatt 200.*

Na. 444

**Mgodi wa Mwadui Kutonufaisha Wananchi**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. SULEIMAN M. N. SULEIMAN)** aliuliza:-

Mgodi wa Mwadui, umekuwepo Kishapu tangu mwaka 1961, lakini haujawanufaisha wana-Kishapu kwa chochote.

Je, kwa nini Serikali, isiamuru Kamati ya Nishati na Madini kutembelea Mgodi huo na kukaa na Viongozi wa Mgodi na kujadiliana jinsi ya kusaidia wananchi wa Kishapu ili wanufaike na rasilimali hiyo iliyoko kwenye maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Mwadui, ulianza uzalishaji kuanzia mwaka 1948. Toka kuanza kwa mgodi huo nchi yetu, imekuwa ikipata faida mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wananchi wa Wilaya ya Kishapu kupata ajira ambapo hadi kufikia mwaka 2012, jumla ya wafanyakazi 1,181 walikuwa wameajiriwa. Huduma za jamii, hususan maji, elimu, afya, ambapo katika kipindi cha mwaka 2010 – hadi 2012, jumla ya shilingi milioni 927 zimetumika.

Fedha za kigeni na mapato mbalimbali ambapo katika kipindi kuanzia mwaka 1999 hadi 2012, Serikali, imeingiza shilingi bilioni 63 kutokana na mrabaha na kodi mbalimbali. Mgodi huo unailipa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu 0.3% ya thamanai ya uzalishaji yaani *Gross Turnover,* ambapo kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Mei, 2013, jumla ya shilingi milioni 280.4 zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeunda *Task Force* kuchunguza mwenendo na mkataba wa *Petra Diamond,* ili kuibana kampuni hiyo kulipa kodi ya mapato. Makampuni yote yenye mikataba na *Petra,* kwa maana ya *subcontractors,* kulipa *Service Levy* kwa Halmashauri ya Kishapu. Tayari *Task Force* hiyo imeshaanza kazi na wakati wowote tutapata ripoti kamili ya mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali, haiwezi kuamuru wala kuituma Kamati ya Kudumu ya Bunge, kwa kuwa sio jukumu lake Kikanuni. Nadhani tutakuwa hatuitendei haki Kamati hiyo na Bunge lako Tukufu kwa ujumla. Ni vizuri Kamati hiyo, ikaachwa kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali badala ya kuitaka ifanye kazi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali, kuhakikisha kuwa mgodi unaleta manufaa kwa wananchi wanaozunguka mgodi huo na hatimaye nchi kwa ujumla, kutokana na mapato stahiki kwa Serikali. Hata hivyo, Kamati ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, itafanya Ziara ya Kikazi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge katika maeneo ya Mtwara, Kishapu katika Mgodi wa Mwadui na Simanjiro katika Mgodi wa *Tanzanite.*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja ya faida ambazo wananchi wanaoishi maeneo jirani ya mgodi wanaweza kupata ni pamoja na kulipwa kwa kodi zao halali. Kumekuwepo na malalamiko kwenye baadhi ya migodi, hasa migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi, kutolipa ushuru wa huduma na suala hili tumelizungumza sana. Nataka tu kujua kwamba, Serikali, imefikia wapi kuwabana hawa wawekezaji, ili waweze kulipa dola milioni 11.15 ambayo migodi wa Bulyanhulu na Buzwagi inadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. ili wananchi

wanaozunguka maeneo ya migodi waweze kunufaika, inahitajika jitihada ya makusudi ya Kiserikali ya kuwajengea wananchi uwezo wa kuweza kutoa huduma. Ili kufanikisha hilo vinatakiwa kujengwa viwanda au Vyuo vya Ufundi kama *VETA* pamoja na miradi ya mikopo midogo midogo kwa akinamama ili waweze kuzalisha mbogamboga na kuuza migodini. Je, Serikali, inafanya juhudi gani za kuwajengea uwezo wananchi wanaozunguka migodi ili waweze kutoa huduma migodini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Maige, kwa jitihada anazozifanya kufuatilia maslahi ya wananchi wake wa Msalala na Kahama kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maige ni shahidi kwamba, Serikali, inafanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba, maslahi ya kodi za kisheria zilizopo katika Halmashauri zetu zinalipwa. Tumefanya Vikao nikimjumuisha yeye mwenyewe na Wajumbe kutoka Wilaya ya Kahama na Mgodi wa *Barrick* na tumebaini upungufu wa malipo ya *Service Levy* ya kiasi cha dola milioni moja ambazo Mgodi wa *Barrick* umeahidi utazilipa haraka, ukiendelea kufanyia kazi kwa maana ya ku-*veryfy* takwimu ama *demand notes* iliyopelekwa na Halmashauri ya Kahama ya dola milioni 11.5 kama alivyozisema.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka katika Bunge lako Tukufu, tulieleza jinsi gani Serikali, inafanya jitihada hizi hata kwenye Halmashauri zingine, ikiwemo Halmashauri ya Geita, ambayo watapata kiwango cha dola milioni 1.4, Halmashauri ya Tarime itapata dola laki sita, Halmashauri ya Nzega wameshapata *2.3 billion* na tunaendelea kufanya jitihada hizo kwa Halmashauri zote nchini ambazo kuna shughuli za uchimbaji, ili waweze kupata kodi zao stahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa eneo hilo la maeneo yanayozunguka migodi, katika mgodi wa *Barrick* wana kitu kinaitwa *Maendeleo Fund. Maendeleo Fund* hii inafanya kazi

ya kuwawezesha vijana kuzunguka kwenye maeneo yanayozunguka mgodi, ikiwemo eneo la Msalala kwenye Mgodi wa Bulyanhulu, kuna Kikosi Kazi cha Wanakijiji ambacho ndio kinahusika na kutoa ajira ndogondogo kama za kufyeka, kufanya usafi, katika Mgodi wa *Barrick Bulyanhulu.*

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote hawezi kupata ajira ndogondogo kama hapitii kwenye kikundi kile ambacho kinaundwa na Serikali ya Kijiji, kinachozunguka Mgodi ule kwa hiyo, jitihada hizi zinafanyika. Vivyo hivyo katika Mgodi wa Tarime, wamefanya hivyo kwenye vikundi vya akinamama ambapo wameweza kutoa eneo la kuponda kokoto kwa ajili ya miradi ya akinamama na vijana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba, *Maendeleo Fund* inaendelea kuwanufaisha vijana wengi na ikiwemo kuhamishia mafunzo ya *VETA* kwenye Mikoa ile yenye migodi na kutoa katika Mkoa wa Kilimanjaro, ambako ilipelekwa huko nyuma. Sasa vijana wengi kwenye maeneo ya mgodi hawapati fursa ya kupata mafunzo haya kwa sababu, *VETA* zilizoko pale hazina mafunzo hayo kwa ajili ya kufanya kazi katika migodi.

**SPIKA:** Naomba tuendelee majibu yalikuwa marefu mno na muda wenyewe unatutupa mkono. Tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwanza ngoja nimwite Mheshimiwa John Cheyo aulize swali la nyongeza.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, leo siku nzuri nashukuru umeniona. Kwanza ni- *declare interest*, natoka sehemu hizo na Mwadui naifahamu. Kwa kuwa Mwadui ni mojawapo ya Migodi ambayo imeonesha kabisa kwamba watu wanaweza kuchimba na mahali wanapochimba wanaachwa hoi kuliko vile walivyokutwa na Mgodi ukafungwa.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri kwamba hili jambo lingeweza kurekebishwa, lakini tunazidi, nchi hii ina kitu kama

Urani, unaichimba, unampelekea mtu mwingine anakuwa *nuclear power,* hivi ni lini nchi hii tutajifunza? Kama hakuna lazima ya kuchimba kwa faida, tuache kuchimba.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza itakuwa ni makosa makubwa sana kuacha kuchimba, hapa kila siku tunaongea bajeti haitoshi, kwa hiyo, tukitaka kuwa na bajeti ya uhakika, ni lazima tutumie madini na tutumie gesi na mafuta tukiyagundua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kodi zinazopatikana na nadhani hiki ni kitu cha muhimu sana watu kuelewa, utasikia watu wanasema bado tunapata mrabaha wa asilimia tatu, siyo kweli, mrabaha wa dhahabu ni asilimia nne, tumetoka tatu tumekwenda nne. Almasi na *Tanzanite* ni asilimia tano, lakini cha muhimu sana na ambayo ni kodi muhimu na ni kubwa ni *corporate tax* ambayo ni asilimia 30. Makampuni mengi sana tumeyabana, yameanza kulipa *Corporate tax.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtu anapoongea mambo ya madini nadhani asing’ang’anie zile asilimia tatu au nne, tumeshatoka. Kingine ambacho wanalipa ni *withholding tax*, ambayo ni kati ya asilimia tano mpaka 15 na isitoshe ndiyo hiyo nyingine ambayo Naibu Waziri amesema, *service levy* ambayo ni asilimia 0.3 ya *turnover.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizo ni kodi, lakini Mheshimiwa Cheyo, Serikali imeamua kuachana na mtindo wa kutegemea kodi peke yake, tunachokifanya sasa hivi ni kwamba, Migodi mipya yote, ni lazima Serikali iwe na hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huko huko ndiko tunakokwenda kwenye mafuta vilevile, tumeanza majadiliano, hata *TPDC* tunataka iingie kwenye biashara na penyewe tuwe na hisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukishapata hisa, ili wananchi wafaidike zaidi, kuna sehemu itabaki Serikalini na kuna sehemu wananchi binafsi wataruhusiwa kununua hisa vile vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukitaka kuboresha pato letu la Taifa liwe kubwa, ni lazima tutumie madini yetu na tusiache kuyachimba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Cheyo, hakuna tatizo lolote, faida ni nyingi zinakuja sasa.

**SPIKA**: Haya tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii.

**Na. 445**

**Utaratibu wa Kulipa Kifuta Jasho kwa Uharibifu wa Mazao**

**MHE. MARTHA M. MLATHA (K.n.y. MHE. DKT. TITUS M. KAMANI)** aliuliza:-

Wakati Serikali ilipojibu swali Na. 74 lililoulizwa na Mheshimiwa Esther L. Midimu, ilitoa taratibu za kufuata ili wananchi walioharibiwa mazao yao na wanyama waweze kulipwa kifuta jasho na kwa sababu wanachi wa Lukungu na Lamadi wametimiza taratibu hizo zilizoainishwa na Serikali:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa kifuta jasho kutokana na uharibifu wa mazao yao uliofanywa na tembo tangu Novemba, 2010?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ina jukumu la kulinda maisha na mali

za wananchi hususan mazao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kufanya doria za msako katika maeneo yanayoathiriwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega, kazi ya kudhibiti wanyamapori waharibifu hufanywa na Vituo vya Idara ya Wanyamapori ya Bunda na Kijereshi kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo yanayoathirika.

Mheshimiwa Spika, orodha ya majina iliyopokelewa katika Wizara inaonesha kuwa wananchi walioharibiwa mazao yao ni wa Vijiji vya Lukungu na Kabita na siyo Lamadi. Katika kipindi cha Novemba, 2010, tembo walivamia vijiji hivyo na kusababisha uharibifu wa mazao ya wananchi 48 katika mashamba yenye jumla ya ekari 51.5.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwatuma Askari wa *KDU*-Bunda kwenda kwenye maeneo ya matukio na kutoa msaada uliohitajika kwa haraka ili kuzuia uharibifu zaidi wa mazao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina utaratibu wa kulipa kifuta jasho kwa uharibifu wa mazao unaosababishwa na wanyamapori. Hata hivyo, kwa kuwa wananchi wa Lukungu na Kabita waliharibiwa mazao yao kabla ya Kanuni za kifuta jasho za mwaka 2011, wananchi hao walilipwa jumla ya sh. 4,050,000/=.

Mheshimiwa Spika, mwisho, fedha za malipo ya kifuta jasho, zilitumwa tarehe 10 Aprili, 2012 kwa Mkuu wa Kanda wa Kikosi Dhidi ya Ujangili Kanda ya Serengeti – Bunda ambaye ailwapa wahusika kwa kushirikiana na viongozi wa Wilaya na Vijiji. Dhumuni la utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba malipo yanawafikia walengwa na kwa uwazi zaidi.

**MHE. MARTHA M. MLATHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na kwamba Waziri amekiri wazi kwamba Askari wale dhidi ya ujangili pamoja na kuzuia wanyama wakali, walikwenda baada ya tukio kuwa limeshatokea. Sasa

naomba nimuulize Naibu Waziri kwamba, je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuimarisha kikosi hicho ili kiweze kuzuia wanyama hawa waharibifu pamoja na ujangili, kabla tukio halijatokea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Mkoa wa Singida tuna pori kubwa sana la Mgori ambalo lina wanyama wengi, waharibifu na wakali, lakini wanaolinda eneo lile ni wanakijiji na ili Askali hawa wa *KDU* waweze kwenda kule ni lazima pori lile liingizwe kwenye utaratibu wa *WMA*. Je, Serikali iko tayari sasa kuingiza pori lile kwenye utaratibu huo ili tuweze kupata Askari hao? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, moja, Serikali inakubaliana naye sana kwamba kazi ya kikosi dhidi ya ujangili imekuwa pana, kwa sababu, moja wanapambana na kuokoa maisha ya wananchi dhidi ya wanyama wakali na waharibifu, lakini hali kadhalika, zoezi lingine jipya limejiongeza la kupambana na vita dhidi ya ujangili.

Mheshimiwa Spika, katika kazi zao za kawaida kikosi hiki kilikuwa kinatakiwa kiwaokoe tu wananchi pale ambapo wanalazimika kupambana au wameingiliwa na wanyama waharibifu kama ambavyo wamekuwa wakifanya. Tumefanya hivyo pale Bunda, tume-*respond* pale ambapo tembo walitoka katika eneo la Kenya na kuingia upande wa Wilaya ya Rombo na kuharibu mazao na kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini kazi kubwa ambayo iko mbele yetu, tunakiongezea nguvu kikosi hiki, tunawaomba wananchi wote washirikiane na Serikali katika vita hii kali dhidi ya ujangili ili tuweze kuokoa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, amegusia juu ya pori la Mgori, pori la Mgori ni kweli lina wanyama, Chuo Kikuu cha Sokoine walifanya utafiti hapo nyuma wakabaini kwamba lina uwezo, kwa maana ya *carrying capacity* ya kuweza kuwa *WMA*. Utaratibu tulio nao katika Serikali, tunawaomba

na tumewasihi wananchi wanaozunguka katika vijiji vinavyozunguka pori hili, waungane, waweze kuyaleta yale maombi rasmi Serikalini na mchakato wa kuweza kuwaruhusu wawe na *WMA,* ni wazi tutakuwa tayari kuwasaidia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Mawaziri acheni kufanya semina hapa, jibuni maswali, aaha!

Na. 446

**Vivutio vya Utalii katika Mkoa wa Mwanza**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Mkoa wa Mwanza una vivutio vingi vya utalii vikiwemo mapango makubwa na mawe yanayoonesha maajabu:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu jiwe linalocheza lililoko katika Kisiwa cha Ukerewe.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Mwanza ni mojawapo ya Mikoa yenye vivutio vingi vya utalii hapa nchini. Miongoni mwa vituo hivyo ni Ziwa Victoria, Miamba ya Mawe yenye kuvutia kama Jiwe la *Bismarck* ambalo limekuwa kama nembo ya kulitambulisha Jiji la Mwanza, Hifadhi za Taifa za Visiwa vya Rubondo na Saanane, Magofu ya majengo ya kale, Makumbusho ya Bujora na Jiwe linaloaminika kuwa linaweza kucheza lililoko katika Kijiji cha Nyamanga katika Kisiwa cha Ukara Wilayani Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na wigo mpana wa kutangaza vivutio vya utalii nchini, pamoja na juhudi mbalimbali za huko nyuma, Wizara yangu kupitia Bodi ya Utalii imeanza kutekeleza mpango wa

kuvitangaza vivutio vya utalii ambavyo vinakabiliwa na changamoto za kufahamika na kufikika kwa kuanzisha jarida mahususi lijulikanalo kama *Hard Venture Tourism* linaloandika taarifa za vivutio kama hivyo nchini.

Mheshimiwa Spika, toleo la kwanza la jarida hili lilitolewa mwezi Agosti, 2012 na lilielezea vivutio vya utalii vya Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mara, Mwanza Kagera na Shinyanga) likiwemo jiwe linaloaminika kuwa linacheza. Jarida hili pamoja na majarida mengine husambazwa ndani na nje yanchi, kwa njia ya machapisho na elektroniki, kwa lengo la kuvitangaza vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kupitia Bodi ya Utalii imefungua Ofisi ya Kanda Jijini Mwanza ili kusogeza huduma za utalii katika maeneo ya Kanda ya Ziwa. Ofisi hiyo itaimarishwa ili huduma mbalimbali za biashara ya utalii zinazotolewa na Wizara zipatikane pale kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa wito kwa uongozi wa Halmshauri za Wilaya husika kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa huduma za malazi na chakula kwa ajili ya Watalii watakaotembelea maeneo hayo.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu yako marefu mno.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nadhani wote waliopita kipindi kilichopita, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongela amelizungumzia sana sana suala hili la jiwe ambalo liko Ukerewe, Kisiwa cha Ukara kwamba, kuna maajabu katika jiwe hili ambalo kweli hucheza likisemeshwa na wale ambao wanatamaduni nalo, lakini jibu la Mheshimiwa Waziri anasema linaloaminika, kwa nini usiamini? Nenda uone maajabu yaliyoko huko ili kusudi useme iliyo kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, hili jarida ambalo linazungumziwa la *Hard Venture Tourism,* naamini limeandikwa kwa Kiingereza, je, kwa nini lisitafsiriwe sasa kwa Kiswahili ili liweze kueleweka, kwa maana vivutio hivi vikubwa vilivyoko Mwanza na kwingine katika Kanda ya Ziwa, kuhamasisha basi utalii wa ndani ambao kila leo Wizara hii huupigia kelele? (*Makofi*)

**SPIKA**: Haya, naomba majibu kwa kifupi. Yako maswali *specific*.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hili jiwe lililopo pale Ukara, katika Wilaya ya Ukerewe linaaminika kwamba lina maajabu na kwa taarifa tulizonazo wakati mwingine watu wamekwenda wameliona likicheza, wakati mwingine wamekwenda wameliona kama halichezi, lakini ukweli ni kwamba ni jiwe linaloaminika kuwa ni la maajabu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua nafasi hii kuwataka Watanzania wote, kwa wale ambao wangependa kushiriki katika kuongeza utalii wa ndani walitembelee, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, lakini tutaendelea kulitangaza jiwe hili na maeneo mengine kama tulivyosema kwenye majibu yetu ya msingi katika maeneo yote ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jarida la *Hard Venture Tourism*, ni kweli matoleo haya mengi ya kitalii, yanaandikwa kwa Kiingereza, lakini tutaagiza kwamba yatafsiriwe pia kwa lugha ya Kiswahili, ili wananchi wengi wapate fursa ya kufahamu na vile vile waweze kutembelea.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa upande wa Mwanza, tuna Kisiwa cha Saa Nane ambacho Serikali

imekipitisha hapa Bungeni kuwa sehemu ya Hifadhi mpya kabisa ya Taifa, na itaupendezesha sana mji wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, tumeagiza *TANAPA* waharakishe kuongeza idadi ya wanyama ambao wamekubaliwa chini ya *carrying capacity* iliyokubaliwa na wataalam, ikiwa ni pamoja na simba, waharakishe kuweka mtaalam mwelekezi ili mipango ya kuweza kuwekeza katika Kisiwa hicho iweze kuwa tayari. Sisi tunaamini kwamba, *the General Management plan* ikikamilika mara moja, itasaidia sana kuongeza wigo wa utalii, katika jiji la Mwanza na sehemu zingine.

**SPIKA:** Haya, Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7); naomba Mwongozo wako, kwa kuwa ndani ya masaa 96 sasa, Kambi ya Upinzani iko wazi, *CUF* inatangaza rasmi kwamba kuanzia sasa kuna mapinduzi ndani ya Bunge, Kambi ya Upinzani inaongozwa na *CUF*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ambayo naomba niinukuu:

"Halikadhalika Mbunge yeyote anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine yeyote anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo

ambalo limetokea mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linafaa, linaruhusiwa, au haliruhusiwi. Kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo ama baadaye kadiri atakavyoona inafaa".

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46 inasema: "Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza, kabla ya muda wa kujibu swali hilo kujibiwa".

Mheshimiwa Spika, wakati lilipoulizwa swali kuhusiana na mambo ya Utawala Bora, ulinipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na nilimuuliza Mheshimiwa Waziri, pale inapotokea Mbunge ameomba ziara *especially* hapa Bungeni, ya Waziri kwenda katika Jimbo husika akiongozana naye na akajibu hivyo kama niko tayari kufanya ziara hiyo hapa Bungeni na kufuatana na Mbunge.

Mheshimiwa Spika, inatokea Waziri anakwenda katika Jimbo bila kumshirikisha yule Mbunge husika na bahati mbaya zaidi, inatokea mara nyingine Waziri anakwenda pale na Mbunge anaonekana yupo pale pale katika mji ule ule, kiasi ambacho wananchi wake wanamdharau na kumwona Mbunge yule hana maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako; jambo hili linafaa Wabunge wako tunadharaulika na wewe upo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaa na Mawaziri wake watatafakari hilo, kwa sababu kwa hakika hata mimi sikuridhika na majibu. Ukimwambia tu Mbunge ninakuja kwako kwani kuna gharama ngapi? Yeye ndiye atakayejua kama anayo nafasi ya kwenda ama hana nafasi ya kwenda. Hivyo ndivyo ilivyokuwa inafanyika miaka yote. Nadhani hilo mtaliona wenyewe kama sasa mmebadilisha utaratibu, lakini ni vizuri Mawaziri mnapokwenda hata kama mtu atashindwa, lakini atasema niliambiwa. Kwa hiyo, mimi nadhani wala tusibishane hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hili suala alilosema Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, kwa mujibu wa Kanuni, Kambi ya Upinzani ni Wabunge wote ambao wako upande mwingine wa Upinzani; yaani siyo Kanuni ya kwetu tu, ni *international* jamani. Tunaendelea kubishana kama ni hivyo siyo hivyo, lakini sisi Kanuni yetu ndivyo inavyosema, ya kwetu ni *international applicable.*

Kwetu sisi nilisema siku za nyuma, tulipoanza mwaka 1995 ndipo tulipoanza Bunge la Kwanza kabisa la Upinzani. Wabunge wa Upinzani wakati huo Kambi kubwa ilikuwa ya *NCCR-Mageuzi* na walikuwa wanajitosheleza. Kwa wakati huo tuliweka *bench-mark* asilimia 30. Mwaka huo wa 1995, *NCCR-Mageuzi,* wali-*meet* hiyo *bench-mark* ya asilimia 30 ndiyo wakawa Kambi ya Upinzani, lakini waliwachukua na wenzao wote. Ilipofika mwaka 2000, Upinzani ulishindwa sana wakawa Wapinzani 26 na siyo asilimia 30 kwa namba, moja, mbili, mpaka 26. Ikaonekana wako mbali kabisa. Ambacho kingeliweza kufanyika ni kwamba, tungeliendelea na Bunge, Wapinzani wapo lakini hakuna Upinzani Rasmi. Busara za Mheshimiwa Spika, aliyekuwepo kwa wakati huo,

akaamua kwamba, itabidi tushushe ile *bench-mark* kutoka asilimia 30 tufanye asilimia kumi na mbili na nusu; na ilikuwa tu ni kwamba, tusingelieleweka, tumefanya Upinzani miaka mitano halafu inayofuata tunaondoa kabisa. Kwa hiyo, tukashusha ile *bench-mark* kutoka asilimia 30 tukapata asilimia kumi na mbili na nusu. Ndiyo tukapata Upinzani, hata kama walikuwa 26, lakini kulikuwa kuna Kambi ya Upinzani, nafikiri wakati ule ilikuwa ni *CUF. (Makofi)*

Ukaja mwaka 2005, ikaonekana *CUF* walikuwa na idadi inayozidi asilimia kumi na mbili na nusu. Kwa hiyo, *automatically* walikuwa wao ndiyo Kambi ya Upinzani, kwa miezi *severally,* wakajidai na wenyewe hivyo hivyo, wakawa wao na hakuna kushirikisha wengine. Kwa busara za Mheshimiwa Sitta, alitumia Diplomasia na Mabalozi wengine kuwaambia, *CUF* wakakubali ku-*incorporate* wenzao katika Upinzani. *(Makofi)*

Ulipofika mwaka 2010, tukaona ile diplomasia aliyoitumia Mheshimiwa Sitta, ilifanya kazi kwa wakati ule lakini kwa sasa haiwezi kufanya kazi, ndiyo maana tuka-*define,* siyo kwamba tulibadilisha; tuli-*define* maana ya *Official Opposition* ni nini. Tulifanya *definition* tu, ilileta maneno na mpaka leo hawaku-*incorporate* wenzao. Mpaka leo wanaendelea wenyewe ndiyo utakuta Kambi Rasmi ya Upinzani ni ya CHADEMA. *CUF* sasa hivi nao wanayo asilimia kumi na mbili na nusu. Hata hivyo, tunachokisema ni kwamba, hawa hawajatoa taarifa kama wameshaacha hii shughuli. Kanuni zetu hazijatoa nafasi kwamba kama wengine hawapo basi wengine wana-*take over immediately.* Kanuni haijasema hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo machache kuhusiana na mwongozo aliouhitaji Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa ninaomba nitangaze kuhusu wageni, hapana naona nianze na matangazo ya kazi kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa James Lembeli – Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii saa 5.00 asubuhi kutakuwa na mkutano wao katika Ukumbi wa Pius Msekwa C; lakini mjue kuna Mkutano wa *TAPAC* pia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba nao watakuwa na kikao saa 5.00 asubuhi, katika Ukumbi Nambari 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, yeye anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Dkt. Muhammed Seif Khatib – Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa 5.00 asubuhi watakuwa na kikao kifupi katika Ukumbi Namba 219, sijui kama wamegongana huko. Kuna mgongano, mtakwenda kuamua wenye huko. Makatibu wenu hawawasiliani. Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 5.00 asubuhi, Ukumbi Namba 133.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* - Mheshimiwa Iddi Azzan, ameomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, Siku ya Jumapili tarehe 23 Juni, kutakuwa na Bonanza kati ya Timu ya *Bunge Sports Club,* Muungano ya Dodoma na *Barafu Jogging Club* kutoka Dar es Salaam. Michezo itakayofanyika ni mpira wa miguu. Mpira wa pete kuanzia saa 10.00 jioni. Asubuhi kutakuwa na matembezi kilometa tano kwa wanamichezo wote. Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuhudhuria bonanza hilo bila ya kukosa na michezo ni afya, michezo pia ni upendo.

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 20 Juni, 2013, pia nilitangaza kwamba, leo jioni saa moja, ninaomba sana pamoja na kwamba mnazo shughuli nyingi, lakini tufike pale tumpongeze Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa kazi alizozifanya katika kipindi cha Bunge lililopita, kutakuwa sherehe katika maeneo ya Bunge. Wengine wanasema hawajapata kadi, ninaomba aliyepata kadi, asiyepata kadi, wote mnakaribishwa. Mnaweza kuja na *partners* wenu mkitaka, mradi wawe watu halali. Hilo ndiyo tangazo, wawe halali na siyo hivi hivi tu. *(Kicheko/Makofi)*

Tangazo lingine ni Mkutano wa *TAPAC.* Tukitoka hapa baada ya chai, kuna Mkutano wa *TAPAC,* ambao utafanyika kwa siku mbili, yaani tarehe 21 Juni, 2013 – 22 Juni, 2013. Sasa ninaomba kuazima masikio yenu. Jana tulifunga suala la Wabunge kujadili Mjadala wa Bajeti. Tulishafunga kuomba maombi ya wachangiaji na tumeiachia nafasi Serikali kujaribu kupata majibu kwa yale tuliyokuwa tumejadili kwa siku hizo tano. Pia tunamtaka Waziri ashirikiane na Kamati ya Bajeti kupitia ule Muswada wa Fedha, kwa sababu baada ya hapo tutaingia kwenye Muswada wa Fedha na watu wengine wanakaribishwa kushiriki kwenye Kamati hiyo ya Bajeti.

Sasa tarehe 24 Juni, 2013, ninaomba hili ninatangaza kwa Serikali na kwa Mawaziri, kama wanasafari warudi, hiyo ndiyo siku tutakayopiga kura. Tarehe 24 Juni, ndiyo siku tutakayopiga kura, Waheshimiwa Wabunge wote isipokuwa waliolazwa hospitalini, mrudi humu ndani. Tarehe 24 Juni, 2013, ndiyo tunapiga kura ya majina. Kwa hiyo, unaitwa jina lako tunaambiwa uko Mtera, watu wako watakuelewa vipi, kwa maana hushiriki hata kushiriki?

Tutakuiteni kwa majina, kwa hiyo, wakumbusheni wenzenu wote. Hiyo ni tarehe 24 Juni, Siku ya Jumatatu. Ninaomba Wabunge wote muwepo na wale wenye safari zao siku hiyo waahirishe kwa sababu ni siku muhimu kwa maana ya maamuzi yetu ya Kiserikali. Kwa hiyo, naomba msikose.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Matumizi Sahihi ya Teknolojia ya Analojia na Dijitali

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 49(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, ninaomba kuwasilisha Kauli ya Serikali kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kuhusu matumizi sambamba ya Teknolojia ya Analojia na Dijitali, iliyowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 21 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka mfumo wa analojia kwenda mfumo wa dijiti: Nchi Wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Duniani, yaani *International Telecomunication Union (ITU),* ikiwemo Tanzania, kwa pamoja ziliridhia kusitisha mfumo wa utangazaji wa runinga unaotumia teknolojia ya analojia na kuanza kuutumia mfumo wa utangazaji unaotumia teknolojia ya dijiti ifikapo tarehe 17 Juni, 2015.

Sababu ya uamuzi huo ni kutokana na faida zinazopatikana kwa kutumia mfumo wa utangazaji wa dijiti ambazo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Ubora wa picha na sauti.

(ii) Ubora wa matumizi ya masafa ya utangazaji, utakaowezesha upatikanaji wa masafa yanayoweza kutumika katika kupanua na kuongeza huduma.

(iii) Matumizi bora ya nishati ya umeme.

(iv) Uwezekano wa kutoa huduma za ziada kama vile *internet* kwenye runinga.

(v) Uwezekano wa kupanuka kwa matumizi ya teknolojia ya runinga za kiganjani na kwenye magari.

Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano hayo, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, zilikubaliana kusitisha mfumo wa utangazaji wa runinga unaotumia teknolojia ya analojia ifikapo tarehe 31 Desemba, 2012 kwa mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa muda wa kutosha kwa nchi wanachama kufanya tathmini ya kiufundi ili kuweza kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza kabla ya kufikiwa kwa tarehe iliyokubaliwa na Umoja wa Mawasiliano Duniani.

(ii) Kuwa na muda mfupi wa kuwa kwenye kipindi cha mpito, ambapo mifumo yote miwili inayotumia teknolojia ya analojia na dijiti inatumika. Hii ni kwa sababu gharama za uendeshaji katika kipindi hiki cha mpito ni kubwa kutokana na vituo kulazimika kuendesha mifumo yote miwili.

(iii) Kutoruhusu nchi zetu kuwa soko la runinga za analojia zilizopitwa na wakati, zinazoweza kuingizwa nchini kutoka katika nchi nyingine iwapo tutachelewa kuzima mitambo hiyo ya analojia.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kabla ya kwenda kwenye mfumo wa dijiti:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukubwa na unyeti wa suala hili hususan jinsi linavyogusa wetu wengi, uhamiaji huo ilibidi kufanywa kwa umakini mkubwa hatua kwa hatua.

Kutekekezwa kwa hatua hizo kumeiwezesha nchi yetu kufikia hatua ya kuingia kwenye mfumo wa dijiti kwa

mafanikio. Ukiliganisha na nchi jirani ambazo bado zinahangaika namna ya kutekeleza mabadiliko hayo kwa hivi sasa wakati ambapo ukomo wa kusitisha utangazaji wa analojia ukiendelea kukaribia.

Hatua zilizotekelezwa ni pamoja na mambo yafuatayo:-

Kwanza, mwaka 2005, Waraka wa Kwanza wa Mashauriano, yaani *Consultative Document* kuhusu umuhimu na faida za kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa analojia kwenda dijiti ulitayarishwa na kufikishwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali nchini. Mwaka 2006 waraka wa pili wa mashauriano na mapendekezo ya muundo wa leseni kwa mfano wa utangazaji wa teknolojia wa dijiti, ulitayarishwa na kusambazwa kwa wadau wote. Mwaka 2007, Kamati ya Kiufundi inayoshughulikia uhamiaji kutoka Mfumo wa Utangazaji wa Analojia kwenda Dijiti iliundwa. Mkutano Mkuu ulijumuisha vituo vyote vya utangazaji nchini ulifanyika kule Bagamoyo, kupitia na kuridhia mfumo wa leseni za utangazaji unaohitajika kwenye mfumo wa dijiti. Mwaka 2010 Kampuni tatu zilipewa leseni za kujenga miundombinu ya kusambaza matangazo kwa mfumo wa dijiti. Kampuni hizo ni pamoja na *Agape Associate Limited, Basic Transmission Limited* na *Star Media Tanzania Limited.*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mabadiliko ya Utangazaji iliundwa. Kamati hii inajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizaa saba. Kamati imeendelea kufanya kazi kwa kukutana angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu, kufanya tathmini na kutoa maelezo ya utekelezaji.

Mwaka 2011, uzinduzi wa Kampeni ya Kitaifa ya kuuelimisha Umma kuhusu mabadiliko ya Mfumo wa Utangazaji uliohusisha Nembo Maalum ulifanywa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 24 Agosti, 2011. Kampeni hiyo ilihusu pamoja na mambo mengine, wimbo mahususi

uliopigwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari wakati wote wa Kampeni hiyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa hatua hizi umefanyika kwa kipindi kirefu cha takribani miaka saba na kuhusisha majadiliano mapana na ya kina ambayo yasingelifanyika kwa wakati, Tanzania isingeliweza kufikia hatua ya kuhamia kwenye mfumo wa dijiti. Ninapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kwa kuwa na mtazamo wa mbali uliotuwezesha kufanikisha zoezi hili. Vilevile ninawashukuru wadau wote hususan Kampuni za Utangazaji ambazo zilitoa ushirikiano wa karibu uliowezesha kufikiwa kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na uendeshaji wa mitambo ya kurusha matangazo ya dijiti: Hatua zilizofikiwa na Kampuni tatu zilizopewa Mitambo ya kurusha Matangazo ya Dijiti ni kama ifuatavyo:-

*(i)* *Agape Associate Limited:* Kampuni hii imefunga mitambo ya dijiti, kwenye Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza. Vilevile inatarajiwa kuwa baada ya miezi mitatu itakuwa imefunga mitambo mingine kwenye Miji ya Iringa, Kigoma, Musoma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

*(ii)* *Basic Transmission Limited:* Kampuni hii imefunga mitambo kwenye Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Kampuni hii imeshaanza kurusha matangazo ya dijiti katika Mkoa wa Dar es Salaam.

*(iii)* *Star Media Tanzania Limited:* Kampuni hii imefunga mitambo ya dijiti kwenye Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza na Tanga. Aidha, baada ya miezi minane inatarajiwa

kukamilisha ufungaji wa mitambo hiyo kwenye mikoa mingine 11.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba niende kwenye hoja za Mheshimiwa Moses Joseph Machali. Hoja yake ya kwanza ilikuwa Wananchi kukosa uwezo wa kununua visimbusi.

Mheshimiwa Spika, kila huduma inayotolewa inaambatana na haki na wajibu wa mtoa na mtumiaji huduma. Ni wajibu wa Wananchi kuhakikisha wanapata habari kwa kununua gazeti, redio au runinga. Ili kuona matangazo ya runinga kwa kutumia mfumo wa dijiti, Mwananchi hana budi kununua runinga yenye uwezo wa kushika mawimbi ya dijiti, ama kuendelea kutumia runinga ya analojia kwa kununua kisimbusi ili aweze kupata matangazo kwa mfumo wa dijiti. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imepunguza makali ya bei za visimbusi kwa kuondoa tozo la kodi ya *import duty.* Wananchi wameendelea kununua visimbusi kwa wingi na ni mategemeo ya Serikali kwamba, ifikapo mwisho wa mwaka huu, Wananchi wengi watakuwa na visimbusi majumbani ili kupata matangazo kwa mfumo wa dijiti.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya uzimaji wa mitambo ya dijiti kwa Jiji la Dar es Salaam: Inakadiriwa kuwa zipo runinga zipatazo 600,00 kwenye Kaya za Jiji la Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2012, zaidi ya runinga 250,000 kati ya 600,000 zilikuwa katika mfumo wa dijiti kupitia teknolojia za kupokea matangazo ya *sattelite* na waya, yaani *cables.* Idadi ya runinga zilizobaki 350,000 ndizo zilizohusika na mabadiliko ya teknolojia kutoka analojia kwenda dijiti. Runinga hizi 600,000 zilizokadiriwa katika Jiji la Dar es Salaam, hazihusishi runinga zilizoko kwenye hoteli, nyumba za starehe na maeneo mengine ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mabadiliko hayo, kati ya Januari, 2012 na Januari, 2013, zaidi ya visimbusi 350,000 vilinunuliwa na Wananchi katika Jiji la Dar es Salaam pekee. Kwa kutumia takwimu za mlinganisho, kati ya runinga

350,000 zilizokadiriwa kuwa katika mfumo wa analojia na visimbusi 350,000 vilivyonunuliwa, inaonesha kuwa zoezi la mabadiliko katika Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla limetekelezwa kwa mafaniko makubwa. Aidha, visimbusi zaidi vinaendelea kusambazwa katika Jiji la Dar es Salaam kutokana na ukweli kuwa baadhi ya runinga ambazo zilikuwa zinapokea matangazo kwa mfumo wa dijiti kupitia teknolojia ya *satellite* na waya, nazo pia zinaweza kutumia visimbusi kupokea matangazo kupitia mitambo ya utangazaji ya ardhini, yaani *terrestrial broadcasting*.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii upo uwezekano wa kuwepo upungufu kiasi kidogo, ambao Mheshimiwa Machali atakuwa ameuona na ambao Serikali inaendelea kuupatia ufumbuzi hatua kwa hatua. Aidha, tathmini ya kina kuhusu utekelezaji wa mabadiliko kwa awamu ya kwanza itafanyika ili kuwezesha kubaini changamoto zilizojitokeza na kuzipatia ufumbuzi kabla ya kuanza awamu ya pili.

Hoja yake ya pili ilikuwa kutopata habari kutokana na eneo husika lililokuwa likifikiwa na mawimbi ya analojia kutokufikiwa na mawimbi katika mfumo wa dijiti. Moja ya vigezo vya kuzima mitambo ya analojia kwenye eneo lolote ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, eneo husika linapata mawimbi ya dijiti. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilipima nguvu ya mawimbi ya dijiti, yaani *signal strength* kabla ya kuzima mitambo ya analojia. Maeneo yote yaliyozimwa mitambo ya analojia yanapata mawimbi ya dijiti kwa zaidi ya asilimia 90. Kwa mujibu wa Kanuni za Umoja wa Mawasiliano Duniani, eneo linatangazwa rasmi kuwa eneo la matumizi ya huduma ya utangazaji iwapo litafikiwa na mawimbi ya utangazaji kwa zaidi ya asilimia 90. Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Moshi, Mwanza na Tanga, inapokea mawimbi ya dijiti kwa zaidi ya asilimia 90, kwa asilimia iliyobaki ambayo mara nyingi ni sehemu za mabondeni au kwenye majengo marefu, watoa huduma wameshauriwa kuweka mitambo midogo ya kuongeza nguvu, yaani *gape fillers* ili kuboresha usikivu. Mfano halisi ni mtambo uliofungwa Makongo Juu katika Jiji la Dar es

Salaam, ambao unasaidiana na mtambo uliofungwa Kisarawe kuongeza nguvu na mwonekano katika maeneo yasiyofikiwa na matangazo hayo vizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ya Mheshimiwa Machali ilikuwa idadi ya mitambo ya dijiti kuwa michache katika kila mji kulinganisha na mitambo ya analojia. Moja ya faida ya teknolojia ya dijiti ni uwezo mkubwa wa kubeba *channel* nyingi za runinga kulinganisha na mfumo wa analojia. Kwenye mfumo wa analojia, safa moja, yaani *frequency* moja la mtambo mmoja wa analojia, hubeba *channel* moja ya runinga wakati safa moja au *frequency* moja la mtambo mmoja wa dijiti linaweza kubeba *channel* zisizopungua 20 za runinga.

Hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Moses Joseph Machali ina upungufu wa maelezo ya kitaalamu kama teknolojia yenyewe inavyohitaji. Hali halisi ilivyo hapa nchini ni kwamba, kwa sasa kuna makampuni au *multiplex operator* watatu, yaani *Agape Associate Ltd, Basic Transmission Ltd, Basic Transmission Ltd* na *Star Media Tanzania Ltd,* ambao walipewa leseni kwa ajili ya kusimika mitambo ya kurushia matangazo ya runinga katika mfumo wa dijiti kama ilivyoelezwa hapo juu. Kila *multiplex operator* mmoja anatakiwa kujenga mtambo katika Mji wa Tanzania na amepewa masafa matatu kwa mtambo huo kwa ajili ya kurusha matangazo ya runinga. Kwa hiyo, kila *multiplex operator* mmoja anaweza kurusha *channel 60* za matangazo ya runinga na kila mji utakuwa na *channel* zaidi ya 180 za matangazo ya runinga kwa kupitia mfumo huu wa dijiti.

Mheshimiwa Spika, faida hii haikuweza kupatikana kwenye mfumo wa analojia. Mlinganisho wa *channel* za runinga za kitaifa zinazopatikana katika miji mbalimbali wakati wa mfumo wa analojia na wakati wa mfumo wa dijiti ni kama ifuatavyo:-

Kwa *channel* ambazo zimepewa leseni za kitaifa ambazo huonesha bure kabla ya uzimaji wa mitambo ya

analojia, Jiji la Mbeya lilikuwa linapata *channel* moja tu ya *TBC*, baada ya kuhamia kwenye mfumo wa dijiti, Jiji la Mbeya kwa sasa linapata *channel* zote tano za bure ambazo ni *TBC1, ITV, Channel 10, Star TV* na *East Africa* TV. Jiji la Tanga kabla ya hapo lilikuwa linapata *channel* mbili tu, yaani *Channel 10* na *TBC1* wakati Jiji la Moshi lilikuwa linapata *channel* mbili tu, yaani *ITV* na *East Africa TV*, Arusha ilikuwa inapata *station* nne, yaani *ITV, Channel 10, TBC1* na *Star TV*. Hivi sasa miji yote hiyo inapata *channel* tano za bure ambazo ni *TBC, ITC, Channel 10, Star TV* na *East African TV* mbali na zile za kulipia kulingana na mahitaji ya mtumiaji. Mitambo ya dijiti bado ina uwezo wa kubeba *channel* nyingi nyingine za ziada.

Hoja yake ya nne Mheshimiwa Machali ilikuwa ni matumizi sambamba ya mifumo miwili ya utangazaji ya analojia na dijiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha Mheshimiwa Machali anapendekeza kuwa na matumizi ya mifumo miwili ya utangazaji kwa kuwasha tena mitambo ya analojia. Serikali ilizima mitambo ya analojia baada ya kushauriana na kukubaliana na wadau wote wakiwemo watoa huduma wa vituo vya runinga. Sababu kubwa zilizosababisha uzimaji wa mitambo ya analojia ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, gharama kubwa ya kuendesha mitambo miwili ya utangazaji, yaani analojia na dijiti kwa wakati wakati mmoja.

Pili, gharama kubwa ya kununua vipuri vya teknolojia ya analojia na ambavyo vinapatikana kwa bei ya juu endapo vitaharibika kwa kuwa vimepitwa na wakati.

Tatu, vituo vya utangazaji kushindwa kulipia gharama za usafirishaji wa matangazo, yaani *transmission fee* kwa mifumo yote miwili (analojia na dijiti), kwa wakati mmoja kwa sababu bado watoa huduma haohao wa vituo vya utangazaji wanagharamia mitambo mingine ya

analojia ambayo ipo mikoa mbalimbali nchini na bado haijazimwa.

Nne, Wananchi kutochukua hatua za dhati kuhamia kwenye matangazo ya dijiti kwa sababu ya kuendelea kuona matangazo kupitia mfumo wa analojia.

Mheshimiwa Spika, aidha, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2013 teknolojia ya zamani ya analojia ilikuwa imesitishwa rasmi katika Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Moshi na Tanga. Hatua hii ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mabadiliko ya teknolojia ya analojia hapa nchini. Hivi sasa Miji ya Kigoma na Morogoro ipo katika majaribio ya urushaji wa matangazo ya dijiti ambayo usimikaji wa mitambo yake ulitekelezwa wakati wa awamu ya kwanza wakati wa uzimaji wa mitambo ya analojia ukiendelea.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya usimikaji wa mitambo ya mfumo wa dijiti itaendelea katika Miji ya Bukoba, Iringa, Lindi, Kahama, Musoma, Shinyanga, Singida, Songea na Tabora. Mitambo ya analojia katika miji tajwa itazima miezi mitatu baada ya kuwashwa mitambo ya dijiti. Mitambo ya dijiti katika miji tajwa inatarajiwa kuwashwa mwezi Septemba, 2013 na itatumika sambamba na teknolojia ya analojia kwa kipindi cha miezi mitatu na baadaye, yaani mwezi Desemba, 2013 mitambo ya analojia itazimwa katika maeneo hayo. Miji mingine iliyobaki itaendelea kutumia mitambo ya analojia hadi pale mitambo ya dijiti itakaposimikwa na kuanza kufanya kazi ili kuwezesha Wananchi wasiofikiwa na teknolojia ya dijiti kuendelea kupokea matangazo ya runinga kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Machali kuwa, duniani kote ni teknolojia tatu tu zinazohusika na kurusha matangazo ya runinga nazo ni *satellite, wire,* yaani *cable* na mitambo iliyosimikwa ardhini. Katika teknolojia hizo, teknolojia ya kurushia matangazo ya runinga kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini ndiyo inahusika na mabadiliko haya ya teknolojia kuelekea kwenye dijiti.

Teknolojia mbili zilizobaki, yaani *satellite* ambayo hutumiwa na Wananchi wengi hasa vijijini na ile ya *wire* inayotumika katika baadhi ya miji, zenyewe kiasilia tayari zipo kwenye mfumo wa dijiti na hazihusiki na mabadiliko yanayoendelea hivi sasa.

Hapa nchini Wananchi walio wengi hasa vijijini wamekuwa wakitumia dishi maarufu kama ungo, kupokea matangazo ya runinga. Hii ni kutokana na matangazo yaliyokuwa yanarushwa kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini kutofika katika maeneo mengi hapa nchini.

Ni matarajio kuwa, mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji nchini kuelekea mfumo wa dijiti, yatawezesha ufikishaji wa huduma za matangazo ya runinga katika sehemu kubwa ya nchi kwa haraka zaidi ukilinganishwa na mfumo wa analojia, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa vipindi vingi zaidi vya runinga.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kufanya jitihada za makusudi, kuwaelimisha Wananchi manufaa yanayotokana na mabadiliko haya. Ninapenda kumsihi Mheshimiwa Moses Joseph Machali pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla, kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuelimisha Wananchi kuhusu umuhimu wa mabadiliko haya ya teknolojia kwa maendeleo ya nchi yetu, kwani mabadiliko ya teknolojia hii ni lazima na hatuwezi kuyaepuka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kama tulivyosema, Mheshimiwa Machali amevamiwa na majambazi. Kufuatana na taarifa tunayopewa ni kwamba, amelazwa Hospitali ya *General* hapa Dodoma na anaendelea vizuri. Kwa hiyo, taarifa hii mkimpelekea itakuwa ni vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda niwatambue wageni tulionao ambao wanatoka Afrika Kusini, nchi rafiki

yetu mkubwa, ni wageni chini ya Wizara ya Habari na Naibu Waziri. Sasa yupo Mheshimiwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais kutoka Serikali ya Afrika Kusini anayeshughulikia utendaji, ufuatiliaji na tathmini katika Serikali hiyo, Mheshimiwa Obert Bapela. Naomba asimame, karibu sana.

Amefuatana na Balozi wa Afrika Kusini hapa nchini, Mheshimiwa Thanduise Henry Liza, karibu sana. Pia yupo na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana katika Ofisi ya Rais wa Afrika Kusini, ambaye ni Dkt. Danis Kilagala, karibu sana. Pia wapo Maafisa wengine ambao amefuatana nao; karibuni sana mjisikie mko nyumbani. Naambiwa wakitoka hapa watakwenda *SUA,* labda na hapa sijui mtawaonesha na vitu kama hivyo, karibuni sana tunafurahi kuwaona. Pia watakwenda kuangalia sehemu zao za kihistoria Mazimbu Morogoro.

Waheshimiwa Wabunge, basi kama nilivyotangaza kwamba, sasa hivi kuna Mkutano wa *TAPAC* na mikutano mingine nimeshatangaza, lakini Jumapili tarehe 23, Wabunge wote wa CCM watakuwa na kikao saa tano katika Ukumbi wa Msekwa, ninyi mko wengi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.51 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Juni, 2013 Saa 3.00 asubuhi)*